



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFJI



Kumb. Na. HA.80/118/01/14

23 Mei, 2023.

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji anapenda kuwatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi ya Msaidizi wa kumbu kumbu daraja la II na Mtendaji wa kijiji daraja la III kwa sifa zifuatazo;-

### 1. Msaidizi wa Kumbukumbu daraja la II – Nafasi mbili (2).

#### 1.1 Kazi za Kufanya.

- Kuorodhesha barua zinazolingia masjala kwenye rejista
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi
- Kusambaza majalada kwa watendaji
- Kupokea majalada yanayorudi masijala kutoka kwa watendaji.
- Kutafuta kumbukumbu/majalada/nyaraka zinazohitajika kwa watendaji
- Kurudisha majaladakwenye kabati la majalada au mahali pengineyanapohifadhiwa.
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya taasisi.

#### 1.2 Sifa za Mwombaji.

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne/sita
- Awe na stahada(NTA Level 6)katika mojawapo ya fani za urasimu ramani(cartography)au(geoinformatics), sheria, Afya au Masjala kutoka vyo vinavyotambulika na serikali wenye ujuzi wa kutumia kompyuta.

#### 1.3 Ngazi ya Mshahara.

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Serikali yaani TGS C/1 kwa mwezi.

---

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, S.L.P 28, Rufiji. Simu: +255 (020)-2010304. Nukushi  
+255 (023) 2010317. Barua pepe: [ded.rufiji@pwani.go.tz](mailto:ded.rufiji@pwani.go.tz). Tovuti: <http://www.rufijidc.go.tz>

## 2. Mtendaji wa Kijiji daraja la III – Nafasi moja (01)

### 2:1 Kazi za kufanya

- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao na kuwa mlinzi wa amani na kusimamia utawala bora katika kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo vijijini
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu
- Kusimamia ukusanyaji wa mapato
- Mhamasishaji wa Umma katika mikakati ya uzalishaji mali, kuondoa njaa na umaskini
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji.
- Afisa masuhuli na mtendaji mkuu wa kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko ya migogoro ya wananchi.
- Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo kijijini.
- Atawajibika kwa mtendaji wa kata
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

### 2:2. Sifa za Mwombaji.

- Kuajiriwa mwenye elimu ya kidato cha nne/sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo; - utawala, sheria, maendeleo ya jamii, Elimu ya jamii, Usimamizi wa fedha na Sayansi ya Jamii kutoka chuo cha serikali za mitaa Hombolo au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 2:3 Ngazi ya mshahara.

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Serikali yaani TGS B/1 kwa mwezi

### **MASHARTI YA JUMLA**

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
2. Waombaji wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45
3. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za wadhamini watatu.
4. Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au waandike namba za NIDA kwenye CV na barua za maombi
5. Waombaji wote waambatishe na Nakala za Vyeti vya Elimu na Taaluma kwa mujibu wa sifa ya kila kada
6. Waombaji waambatishe na nakala za cheti cha kuzaliwa
7. Maombi yaambatishe na picha mbili za rangi (pass port size) zilizopigwa hivi karibuni
8. Result slip, statement of Result, testimonial hazitakubaliwa

---

Halmashauri ya Wilaya Rufiji, S.L.P 28, Rufiji. Simu: +255 (020)-2010304. Nukushi  
+255 (023) 2010317. Barua pepe: [ded.rufiji@pwani.go.tz](mailto:ded.rufiji@pwani.go.tz). Tovuti: <http://www.rufijidc.go.tz>

9. Waombaji ambao ni watumishi wa Umma wapitisha maombi yao kwa waajiri wao wa sasa
10. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka baraza la mitihani la Tanzania
11. Maombi yote yatumiwe kwa njia ya posta kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 28,  
**UTETE/RUFIJI**

Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya mkono hayatapokelewa.

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 05.06.2023 saa 9:30 Alasiri.

**Imetolewa na:**



Sebastian L Gaganija.  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
RUFUJI.**

**Nakala:**

- Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S.L.P 2320,  
**DODOMA.**
- Mbao zote za Matangazo

---

Halmashauri ya Wilaya Rufiji, S.L.P 28, Rufiji. Simu: +255 (020)-2010304. Nukushi  
+255 (023) 2010317. Barua pepe: [ded.rufiji@pwani.go.tz](mailto:ded.rufiji@pwani.go.tz). Tovuti: <http://www.rufijidc.go.tz>